# OSEA KOLINISAU




# CHANZO CHA FURAHA YANGU YOTE

Kufikia mahali nilipo katika taaluma yangu ya raga iligharimu bidii na mazozi mengi. Ninashukuru kwa mafundisho yote na msaada wa baba yangu. Kama mchungaji, baba yangu alinifundisha kuwa kwa kufanya kazi kwa bidii na kuwa na imani katika Yesu Kristo, hakuna lisilowezekana. Nimeona hayo yakifanikiwa katika maisha yangu. Ninajua kwamba ni Kristo ndiye alinipa talanta yangu na ninashukuru kwa fursa Alizonipa ili kuitumia kwa utukufu Wake.

Kuelekea Olimpiki ya Rio ya 2016 kulikuwa kwa kushangaza. Waliponiambia kuwa mimi ndiye nitakayepeperusha bendera ya nchi yetu, lilimaanisha sana kwangu. Wakati wowote nilipokuwa nikitazama sherehe ya ufunguzi wa Olimpiki kabla ya hapo, ningeangalia miangaza, wanariadha wote wakitoka nje, na bendera ambazo ziliwakilisha nchi nyingi. Kujua nitaitembeza bendera hii katika moja ya hafla kubwa zaidi ya michezo ulimwenguni lilinifanya niwe na msisimko. Raga ni mchezo nambari 1 wa kimataifa wa Fiji. Nilijivunia kuweza kuwakilisha sio mimi tu na timu yangu, bali familia yangu na nchi yangu pia. Hii ilikuwa heshima kubwa.

*__Osea Kolinisau__ ni mchezaji stadi wa raga wa Fiji aliyeipeperusha bendera ya nchi yake kwenye Olimpiki ya Rio ya 2016. Alikuwa pia nahodha wa timu ya wachezaji saba ya Fiji na kuiongoza kwenye medali ya dhahabu - medali ya kwanza kabisa ya Fiji kwenye Michezo ya Olimpiki. Kolinisau anacheza kitaalam kwenye Ligi Kuu ya Raga nchini Marekani.*

Picha za AP / Kamran Jebreili, Themba Hadebe

# "Kabla sijazaliwa, BWANA aliniita, kutoka katika tumbo la mama yangu, amelitaja jina langu." - Isaia 49: 1





Kuwa kwenye Olimpiki kuliniletea kiwango kipya kabisa cha furaha. Hapo awali, nilikuwa nikilia kila wakati wimbo wetu wa taifa ulipochezwa. Lakini kwenye Michezo ya Olimpiki, sikuweza kujizuia bali kutabasamu.

Watu wangeniuliza, "Kwa nini unatabasamu sana?" Na singeweza kujibu. Nilitaka tu kucheka kwa sababu ya furaha iliyokuwa ikibubujika ndani yangu.

Lakini jambo hata kubwa zaidi kuliko nafasi ya kuwakilisha nchi yangu ni fursa niliyonayo ya kuwakilisha Ufalme wa Mungu. Hakuna kinacholinganishwa na hilo! Unaweza kushinda medali ya dhahabu, lakini tuzo kubwa zaidi ni kujua ya kwamba wewe ni mtoto wa Mungu. Lengo kuu kwa mtu yeyote linapaswa kuwa kumjua Yesu kama Bwana na Mwokozi wake wa kibinafsi.

Mungu hunipa furaha niliyonayo kwa mchezo wa raga. Yeye ndiye chanzo cha furaha yangu yote. Kuwa na Kristo ndani yangu, ninapata amani na utulivu usioweza kuelezeka. Mimi na wanatimu wenzangu tunahakikisha tunafanya sala na kuwa na wakati na Mungu kabla na baada ya kila wakati wa kucheza. Kila asubuhi, tunafanya ibada pamoja na tena baada ya kufanya mazoezi pamoja. Sote tunajua kwamba Yesu Kristo ndiye sababu yetu sisi kucheza mchezo huu. Yeye ambaye alituokoa kutoka mautini na kutuleta uzimani kwa njia ya kifo na ufufuo wake yuko upande wetu.

Ninapomaliza kucheza raga, ninatumai kuwa watu wataangalia nyuma, wataona jinsi nilivyocheza na kugundua kuwa nilikuwa tofauti — sio kwa sababu ya kile nilichofanya, lakini kwa sababu ya Yule Ninayemwamini. Watu wakiona niliko leo, ninataka wajue nimefika hapa kwa sababu ya Kristo peke yake.

Bila Kristo maishani mwangu, singekuwa mtu niliye leo. Nisingeshinda medali ya Olimpiki. Nina furaha ya kwamba Mungu alinichagua kushindana na kushinda, lakini ninafuraha hata zaidi kuwa mimi ni sehemu ya Ufalme Wake, ulio na thamani kubwa kushinda dhahabu.

